**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 8, Issue 1, 2025**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii

*Oroko Kerubo Judith[1*] na Dkt. Jesse Joseph Muriithi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: jorosh1994@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*20 Mei 2025*

**Istilahi Muhimu**:

*Vitabu vya Kiada, Ufundishaji, Ujifundishaji na Umaizi.*

## IKISIRI

Mandhari ni kipengele muhimu sana katika kazi yoyote ile ya fasihi na nyimbo hazijasazwa. Madhumuni makuu ya makala haya ni kueleza kuhusu usawiri wa mandhari katika nyimbo teule za jadi za jamii ya Abagusii. Yaani kuonyesha maudhui yaliyojengwa kupitia kwa nyimbo teule, kudhirisha mila na desturi ambazo zinaangaziwa kupitia kwa nyimbo hizo na hata kuonyesha uhusiano kati ya jamii na mazingira anamoishi. Mandhari ambamo nyimbo hizi zilikuwa zimejikita yalikuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha uwasilishaji wa nyimbo husika. Katika kazi yoyote ya fasihi, mandhari yana nafasi muhimu sana. Kwanza, watunzi wanaweza kujenga maudhui ya kazi zao kwa kutumia. Pili, dhamira na toni ya kazi husika inaweza kukuzwa. Hali kadhalika, usawiri wa wahusika unaweza kudhihirishwa kikamilifu na mwisho kabisa matumiza mbinu mbalimbali za mtindo yanaweza kuendelezwa.

**APA CITATION**

Oroko, J. K. & Muriithi, J. J. (2025). Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii. *East African Journal of Swahili Studies, 8*(1), 339-347. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

**CHICAGO CITATION**

Oroko, Judith Kerubo and Jesse Joseph Muriithi. 2025. “Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii”. *East African Journal of Swahili Studies* 8 (1), 339-347. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

**HARVARD CITATION**

Oroko, J. K. & Muriithi, J. J. (2025) “Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii”, *East African Journal of Swahili Studies*, 8(1), pp. 339-347. doi: 10.37284/jammk.8.1.3020

**IEEE CITATION**

J. K., Oroko & J. J., Oroko “Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii”, *EAJSS*, vol. 8, no. 1, pp. 339-347, May. 2025.

**MLA CITATION**

Oroko, Judith Kerubo & Jesse Joseph Muriithi. “Usawiri wa Mandhari katika Nyimbo Teule za Jadi za Jamii ya Abagusii”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 1, May. 2025, pp. 339-347, doi:10.37284/jammk.8.1.3020.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

## UTANGULIZI

Dhana ya mandhari imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Kulingana na Njogu na Chimerah (2008) mandhari ni kama mazingira ya wahusika pamwe na matukio na inahusu wanamokaa wahusika na kuingiliana. Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari ni mahali na wakati ambapo tukio au hadithi husimuliwa. Mahali hapa hurejelea mazingira ya kijiografia, kitamaduni na thamani na hata mawazo ambayo yanatawala mazingira yenyewe. Kwa upande mwingine Mbatia (2001) anasema kuwa mazingira yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Ni sura ya mahali hasa ikiwa yavutia. Naye Muusya (2012) akimnukuu Moss (1987) hayatofautiani na wataalamu wengine, anasema kuwa ni mahali ambapo hadithi hutokea. Huweza kuwa moja au ikabadilika. Mandhari huwa ni muhimu sana katika kuelewa hadithi. Anaendelea kusema kuwa watu ni sehemu ya mandhari.

Mbali na hayo, Hassan (2024) anaeleza mandhari katika fasihi kama muktadha ua mazingira ambayo hadithi au kazi ya fasihi inasimikwa. Anaendelea kusema kuwa ni maelezo ya mahali, wakati, hali ya hewa, utamaduni na mambo mengine yanayotoa mazingira ya kazi za fasihi. Mandhari husaidia kuwapa wasomaji au wasikilizaji taswira ya kina na hisia ya mazingira ambayo hadithi inatendeka. Kutokana na maelezo haya ya wataalamu mbalimbali, mandhari ni mazingira ya kiwakati, mahali na hali ambamo matukio ya fasihi na wahusika wa fasihi hupatikana. Mandhari yanaweza kuwa halisi, mandhari ya kihistoria, mandhari ya kijiografia na mandhari ya hali. Katika nyimbo za jadi, watunzi walitumia mandhari mbalimbali katika kufanikisha uwasilishaji wa nyimbo husika. Mandhari kama vile: jandoni, sherehe za ndoa, sherehe za mazishi, sherehe za kuzaliwa kwa watoto na shambani yalitumiwa.

Makala haya yanalenga kufafanua jinsi ambavyo mandhari ya jandoni yalitumiwa kuwafunza wavulana kuhusu kungwi za utu uzima, matarajio ya jamii kwao na hata kusawiri uhusiano katika ya jamii ya Wakisii na majirani zao kama vile Wakalenjin na Wamaasai. Hali kadhalika yanaonyesha mchango wa mandhari katika kuendeleza nyimbo za ndoa ambapo mandhari haya yanatumiwa kuwatayarisha wanandoa kuhusu mambo watakayokumbana nayo katika taasisi hiyo. Katika nyimbo za mbolezi mandhari hayo yalikuwa na nafasi muhimu katika kujenga maudhui ya nyimbo hizo kama vile taasubi ya kiume na hata kuonyesha imani ya jamii kuhusu kifo. Mandhari pia yamedhihirishwa kuwa na mchango mkubwa katika kuonyesha thamani ya watoto hasa wa kiume katika jamii hii. Mwisho kabisa katika mandhari ya shambani makala haya yalilenga kuounyesha umuhimu wa kutia bidii hasa shambani kwa sababu mtu yeyote aliyekuwa mvivu alikuwa anadharauliwa na wanajamii.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Uliendelezwa maktabani ambapo watafiti walisoma kazi ambazo zimeandikwa na wataalamu mbalimbali kuhusu mandhari. Hali kadhalika, utafiti huu uliendelezwa nyanjani ambapo data ya kimsingi ilipatikana. Walizirekodi nnimbo hizo kwa simu ya rununu na kupiga picha kisha wakachanganua baadaye kwa kuongozwa na malengo utafiti. Mtafiti alisaili watu mbalimbali kuhusiana na nyimbo za jadi. Kwanza alisaili watu wakongwe wawili (mmoja wa kike kwa jina Mary Nyakerario na mwingine wa kiume kwa jina James Maoga), hadhira ambapo alisaili watu wawili wawili katika kila sherehe kisha akawasaili waimbaji wawili wawili wa kila sherehe katika jamii teule. Nyimbo ambazo zilikuwa ni msingi wa utafiti zilikuwa ni tisa. Ambapo wimbo wa kwanza ni wa jandoni (‘*Obeire Omomura’: Amekuwa* Mwanamume), wimbo wa pili na wa tatu ni ndoa (‘*Abagusii Bakabora’*: Wakisii Wakasema, ‘*Nkaancha Konywoma’* :Nikakubali Kuoa) wimbo wanne na wa tano ni mbolezi (‘*Makweri*’: Kifo ‘*Tiga Korea*’: Usilie). Wimbo wa sita na saba ni kuzaliwa kwa mtoto (*‘Sindigisa’*, ‘*Eng’enang’eni Yabarire*’: Nyota Imeng’aa) kisha wimbo wa nane

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

na tisa ni kazi hasa shambani(‘*Renda Rigesa*’: Tunza Mavuno), ‘*Obori Bwa Baba’: Wimbi* Jameni).

## MANDHARI KATIKA NYIMBO ZA JADI

### Mandhari ya Jandoni

Jando ni mahali ambapo watoto wa kiume huenda kutahiriwa na kufunzwa mambo ya utu uzima. Katika wimbo wa ‘*Obeire Omomura’* (Amekuwa Mwanamume) mandhari ya jandoni yalitumiwa kuonyesha mabadiliko ambayo mvulana huyo ameshuhudia. Kabla ya kuingia jandoni mvulana huyo alichukuliwa kama mtoto mdogo ambaye hakuwa anajifahamu wala hakuwa anaheshimwa na wanajamii ila baada ya kudhihirisha ujasiri katika mchakato wote wa jandoni kijana huyo alidhihirisha kuwa yeye ni mwanamume. Mwanamume ambaye ni jasiri na aliyestahili kuheshimiwa na wanajamii wote. Kutokana na mabadiliko hayo, mama yake alionywa dhidi ya kumpa majukumu ambayo yalichukuliwa kuwa ni ya wanawake au ya wavulana ambao hakuwa wametahiri kama vile kuenda mtoni kuteka maji au kuteka kuni. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Obeire omomura* | *Amekuwa mwanamume* |
| *Ng’ina amosike* | *Mama yake amheshime* |
| *Tamotoma roche* | *asimtume mtoni* |

Hali kadhalika, mandhari hayo yalidhihirisha uhasama na mzozo uliokuwa kati ya jamii ya Abagusii na majirani zao ambao ni jamii ya Abamanyi (Wamaasai) na Wakipsigis. Kulingana na Galtung (1969) anaeleza mzozo kama mchakato wenye nguvu ambapo muundo, mtazamo na tabia zinazidi kubadilika na kupelekea watu kuathirika. Hali kadhalika, Wall (1985) anasema ni mchakato ambapo makundi mawili au zaidi yanajaribu kuzuiana katika kuafikia malengo yao. Anaendelea kusema kuwa mambo yanayochangia katika mzozo ni kutegemeana, tofauti za malengo na mitazamo tofauti. Hivyo basi, mzozo ni hali ya watu wawili au makundi mawili au zaidi kutoelewana kwa sababu ya tofauti zao za kiimani, kitamaduni, kiuchumi, malengo tofauti na uhaba wa raslimali. Kupitia kwa mandhari hayo, wavulana hao waliambiwa wawe tayari kuenda kupigana na maadui wao ili kurejesha mifugo ambao walikuwa wameibwa. Vijana hao waliaminiwa kuwa walikuwa jasiri na hatari kwa sababu walirejelewa kama chatu. Neno chatu lilitumiwa kijazanda katika kuwarejelea vijana hao. Wanajamii walitahadharishwa dhidi ya kuwafanyia mzaha. Waliambiwa kuwa iwapo kuna yeyote aliyekuwa anashuku, angejaribu kuwachokoza ili ashuhudie ukali wao. Kulingana na TUKI (2019) chatu ni nyoka mkubwa na mnene anayeua kwa kujiviringisha kwenye mwili wa windo lake kwa nguvu. Kutokana na sifa za vijana hao, jamii iliwapa nafasi ya kudumisha usalama kijijini. Wanajamii waliambiwa wawatayarishie silaha za vita kama vile mkuki na ngao. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Aturerigwe ritimo* | *Anolewe mkuki* |
| *Nanguba boigo* | *Na ngao pia* |
| *Abamanyi batochandire kera engaki ee-yoo* | *Wamaasai wametusumbua kila wakati ee-yoo* |
| *Abasigisi batosamirie ee-yoo* | *Wakipsigis wametuibia ee-yoo* |
| *Banto aba bairire chitugo chiato ee-yoo* | *Watu hawa wamechukua mifugo wetu ee-yoo* |
| *Oyotaegenetie tiga ache kwerorera ee-yoo* | *Asiyeamini wacha aje ajionee ee-yoo* |
| *Kwerorera enyamweri korwa engoro ime ee-yoo* | *kujionea chatu kutoka shimoni ee-yoo* |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

**Sherehe ya Ndoa**

Katika wimbo wa '*Abagusii Bakabora'* (Wakisii Wakasema), mandhari haya yalikuwa na mchango mkubwa sana. Wanandoa walipewa nasaha kuhusu maisha ya ndoa. Nasaha ni mwongozo au mawaidha ambayo mtu hupewa kuhusu hali fulani. Wanandoa waliambiwa kuwa jukumu lao kuu lilikuwa ni kupata watoto. Walikumbushwa kuwa ili jamii iwaheshimu, ilikuwa ni lazima kupata watoto kwa sababu yeyote ambaye hakuwa na mtoto alirejelewa kama mti mkavu. Katika jamii yetu hasa kwa wakulima, mti au mmea wowote ambao umekauka au ni mkavu hauna faida yeyote hivyo basi wao huishia kuukata. Wanandoa walitahadharishwa dhidi ya kuwa mti mkavu. Kwa upande mwingine, familia ambayo ilijaliwa na watoto ilichukuliwa kuwa ni familia ambayo ilikuwa imebarikiwa kwa sababu watoto hao wangechangia katika kukiendeleza kizazi cha wazazi wao, wangewasaidia katika kufanya kazi hasa za shambani na pia watoto wavulana wangechangia katika kudumisha usalama. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Abagusii bakare bagakwana* | *Wakisii wa kitambo walinena* |
| *Bagakwana bagateba ng'a* | *Wakanena wakasema kuwa* |
| *Oyotabwati mwana no'mote mwomo* | *Asiye na mtoto ni mti mkavu* |
| *Oyobwate omwana okboko kwaye gwaichoire* | *Aliye na mtoto mkono wake umejaa* |

Hali kadhalika, mandhari hayo yalitumiwa kuwasisitizia umuhimu wa kufanya kazi. Katika sherehe hizo, walihimizwa kushirikiana katika kufanya kazi hasa za shambani kwani watu wavivu hawakuwa na thamani yoyote kwenye jamii. Tabia ya umbeya ambayo ilikuwa maarufu miongoni mwa wanawake ilisutwa ilikashifiwa vikali katika mandhari hayo kwa sababu iliaminiwa kuwa umbeya uliwafanya wanawake wengine wawe wavivu na kukosa kutenga muda wa kufanya kazi hivyo basi kuchangia katika kuteseka kwa familia zao. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Omaiya chingero bonnyangero* | *Binadamu aliyekamili anaimba na kuimba* |
| *Omokungu sioma siomi nkayi akomanya* | *Mwanamke anayependa kuzurura anajua aje* |
| *Nkayi akomanya bwarugirwe aegwe obokombe* | *Anajuaje kumepikwa apewe jembe* |

Mandhari haya pia yalisawiriwa katika wimbo wa '*Nkaancha Konywoma'* (Nikakubali Kuoa) ambapo wanandoa walionywa dhidi ya kuomba au kutoa talaka. Wawili hao walihimizwa kuiheshimu taasisi ya ndoa na kujaribu juu chini ili ndoa yao isisambaratike. Mwanandoa yeyote aliyetoa talaka au aliyeitisha talaka alichukuliwa kuwa msikwao hivyo basi alifukuzwa kutoka kwenye jamii kwa sababu alichukuliwa kuwa amewakosea mababu heshima. Kutokana na onyo hili, wanandoa walijifunza umuhimu wa kuvumiliana na walitafuta ushauri nasaha kutoka kwa watu wenye hekima na maarifa kuhusu ndoa ili kuizuia ndoa yao kusambaratika. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Nkamoseria genda! Genda! Ee nkamoseria pi!* | *Nikamfukiza enda! Enda! Ee nikamfukuza kabisa* |
| *Agantebia oikire tari kogenda ande pi* | *Akaniambia amefika haendi mahali kabisa* |
| *Abanto bakabora ee negesaku gekabora* | *Watu wakanena ee na ukoo ukanena* |
| *Kwabeire kironchi yara kironchi otarochi* | *Umekuwa msikwa cheza msikwa usipochunga* |
| *Nkorutwa orwe omwaro otabwati omochi ande* | *Utatupwa kama tendeguu lisilo na kwao* |

 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 8, Issue 1, 2025
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

**Mandhari ya Mazishi/Maombolezo**

Kulingana na Hakola (2014) kifo ni tukio lisiloepukika lakini ni la kushangaza. Kifo ni zaidi ya uzoefu wa kimwili au kisaikolojia katika kuhusu ubinadamu na usimulizi wa hadithi. Katika wimbo wa '*Makweri*' (Kifo) mazingira ya mazishi yamekuzwa kwa kina. Kwanza, idadi ya vifo kwenye jamii ilikuwa inongaezeka ikilinganishwa na siku zilizotangulia. Watu walikuwa wakiaga dunia kila wakati jambo ambalo liliwafanya wanajamii kuhuzunika sana. Katika kusisitiza kuongezeka kwa vifo, mtunzi alisema kuwa kifo kilikuwa kinapitia kwenye milango, kwenye dirisha na hata kwenye paa. Hali kadhalika, mandhari hayo yalitumiwa kuonyesha kuwa kifo hakikuwa na ubaguzi wowote. Kilikuwa kinavamia mtu yeyote kwenye jamii. Katika jamii, watu wa tabaka la juu wanaheshimiwa na kuogopwa na kila mtu, ila kutokana na mandhari haya ilikuwa wazi kuwa kifo hakikuwa kinamwogopa wala kumsaza mtu yeyote. Awe ni mtoto, awe ni kijana, awe ni mzee, tajiri, maskini au kiongozi. Kifo kilikuwa kimewaweka watu hawa kwenye chungu kimoja. Kila mtu kwenye jamii alikuwa na hofu ya kufa au kuathiriwa na kifo kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Makweri aeteire emerango* | *Kifo kimepitia kwa milango* |
| *Makweri aetire chitirisa* | *Kifo kimepitia kwa dirisha* |
| *Makweri aeteire ebirama* | *Kifo kimepitia kwa paa* |
| *Akoira abanto ebitongo* | *Kinawapeleka watu pabaya* |
| *Makweri tamanyeti omogoka* | *Kifo hakijui mzee* |
| *Makweri tamanyeti omong'ina* | *Kifo hakijui mama* |
| *Makweri tamanyeti abana* | *Kifo hakijui mtoto* |
| *Akoira abanto ebitongo* | *Kinawapeleka watu pabaya* |
| *Makweri tamanyeti omotaka* | *Kifo hakijui maskini* |
| *Makweri tamanyeti omonda* | *Kifo hakijui tajiri* |
| *Makweri tamanyeti omorai* | *Kifo hakijui kiongozi* |
| *Akoira abanto ebitongo* | *Kinawapeleka watu pabaya* |

Kando na hayo, katika wimbo wa '*Tiga Korea*' (Usilie), mandhari yake yalitumiwa kujenga taasubi ya kiume. Hali hii ilidhihirika kwa sababu wanaume walionywa dhidi ya kuonyesha hisia zao hasa za huzuni. Waliambiwa kuwa, mwanamume hakupaswa kulia, jamii iliamini kuwa machozi ya wanaume ambao kwa wimbo huu walirejelewa kama fahali hayakupaswa kuonekana kwa sababu yangeonekana ingekuwa ishara ya unyonge. Kwa upande mwingine mwanamke alisawiriwa kama kiumbe ambaye ni mnyonge. Kinyume na ilivyokuwa kwa wanaume, wanawake walikuwa na uhuru wa kulia kadri ya uwezo wao kwa sababu iliaminiwa kuwa hawakuwa na uwezo wa kufumbika hisia zao ikilinganishwa na wanaume. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *Aye ise Kwamboka tiga korera gaki* | *Wee baba mtoto wacha kulia jameni* |
| *Amakweri namaroro amakweri nkare achete* | *Kifo ni kichungu kifo kilianza kitambo* |
| *Mariga yechiheri tarikororekana pi* | *Machozi ya fahali hayaonekani kabisa* |
| *Remereria remereria Nyasae nabae abanda* | *Vumilia vumilia Mungu atawapa wengine* |

Hali kadhalika, utamaushi uliotokana na wazazi kufiwa na mtoto wao ulidhihirika. Katika familia moja ulikuwa unapata idadi kubwa ya watoto, wengine walikuwa wanapata watoto hata zaidi ya kumi. Ingawa walikuwa na idadi kubwa ya watoto, kila mmoja wao alikuwa na nafasi muhimu sana katika familia hiyo. Kando na hilo, kila mtoto alikuwa na upekee wake, hivyo basi mtoto mmoja alipoaga dunia, aliacha pengo kubwa sana ambali halingeweza kuzibwa na mtu yeyote yule. Jambo

 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

hili liliwahuzunisha wazazi sana kwa sababu waliamini kuwa mzazi hastahili kumzika mtoto wake ila mtoto ndiye anastahili kumzika mzazi wake. Kwa mfano:

*Ng'ai ndarusie omwana onga Kwamboka*
*Ng'ai ndarusie omwana onga Kwamboka*
*Kwamboka ototigire ochire notana korera*
*Baba ng'ina omwana notana korera okure*

*Nitatoa wapi mtoto kama Kwamboka*
*Nitatoa wapi mtoto kama Kwamboka*
*Kwamboka ametuacha hata usilie*
*Mama mtoto hata uslie amekufa*

**Sherehe ya Kuzaliwa kwa Mtoto**

*'Sindigisa'* ni wimbo ambao uliimbwa baada ya mtoto kuzaliwa. Mandhari ya wimbo huu yalionyesha furaha ambayo ukoo na jamii ilikuwa nayo baada ya mama kujifungua salama. Walimpongeza mama kwa kuwapa mtoto. Pili, walimpongeza kwa kuitunza mimba kwa miezi tisa na kuhakikisha kuwa mtoto alikuwa na afya bora. Wanajamii walielewa kuwa kipindi cha uja-uzito kilikuwa ni hatari kwa mama na kwa mtoto pia na ndio sababu walirejea kipindi hicho kama kuwa juu ya mti kauli ambayo waliitumia kijazanda. Basi, kumwona mama na mtoto wakiwa na afya bora ilikuwa ni vigumu kwao kuificha furaha yao. Kulingana na WHO (2024) wanasema kuwa katika mwaka wa 2020 karibu wanawake 800 walikufa kila siku kutokana na sababu zilizoweza kuzuilika zilizohusiana na ujauzito na kuzaa. Wanaongezea kwa kusema kuwa kifo cha mama mjamzito kilitokea kila dakika mbili mnamo mwaka wa 2020. Kutokana na takwimu hizi za Shirika la Afya duniani, furaha ya wanajamii hawa ilieleweka ingawa ilikuwa katika jamii ya jadi.Kwa mfano:

*Nyaboke orure omote igoro*
*Ekiomoyo omwana otoeire*
*Ee sindigisa ee baminto*
*Oiboirwe omwana omoke*
*Baminto rero nmogoko ee omogoko*

*Nyaboke ametoka juu ya mti*
*Cha moyo na mtoto ametupa*
*Ee sindikiza watu wetu*
*Amezaliwa mtoto mdogo*
*Watu wetu leo ni furaha ee ni furaha*

Hali kadhalika, wimbo wa '*Eng'enang'eni Yabarire*' (Nyota Imeng'aa) yalisawiri mandhari kwa njia nyingine ya upekee. Wimbo huu ulijikita katika mandhari ambamo mtoto wa kiume alizaliwa. Katika jamii hii, mtoto wa kiume alikuwa na thamani kubwa ilipolinganishwa na mtoto wa kike na ndio sababu mtoto huyo alirejelewa kama 'Nyota'. Mtoto huyo iliaminiwa kuwa baada ya kukomaa angeisaidia familia na jamii sana. Kwa mfano: angeenda kupigana kwa niaba ya jamii yake, angedumisha usalama bomani mwao na pia angechangia katika kuendeleza kizazi cha wazazi wake. Kupitia kwa wimbo huu, jamii iliambiwa ije ishuhudie baraka hiyo na pia wajiunge na familia ya mtoto huyo katika kusherekea kuzaliwa kwa mtoto huyo. Kwa mfano:

*Eng'enang'eni yabarire eee yabarire x2*
*Omonto bweng'encho oikire, ee oikire x2*
*Korwa mocha inchwo morore, ee morore x2*
*Korwa maate inchwo mwerorere, ee mwerorere x2*

*Nyota imeng'aa, ee imeng'aa x2*
*Mtu wa maana amewasili*
*Kutoka Kaskazini njoo muone. Ee muone x2*
*Kutoka chini njo mjionee, ee mjionee x2*

**Mandhari ya Shambani**

Mojawapo ya shughuli ya kiuchumi ambayo jamii hii ilishiriki ilikuwa ni kilimo. Walijishughulisha na kilimo cha ndizi, njugu, maharagwe, viazi vitamu, wimbi, mihogo na viazi vikuu. Katika wimbo wa '*Renda Rigesa*' (Tunza Mavuno), mandhari ya shambani yalitumiwa kuwaonyesha matunda ya bidii yao. Wakulima walikuwa wanaambiwa kuwa mazao yao yaliyokuwa shambani yalikuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

yamenawiri hivyo basi walistahili kujitayarisha kwa ajili ya mvuno. Hali kadhalika, walikumbushwa umuhimu wa kuhifadhi vyakula vyao vizuri ili viwafae kwa siku za usoni. Walikumbushwa kuhusu madhara ya njaa iliyo wavamia ambapo watu na mifugo wengi walipoteza maisha yao. Kando na hayo, mandhari hayo yalitumiwa kuonyesha usaliti wa viongozi wao ambao waliwaruhusu vijana na watu wenye nguvu kutekwa nyara ili kuenda kushiriki kwenye Vita vya Kwanza vya Dunia na wengine wakaenda kufanya kazi kwenye mashamba ya wazungu. Usaliti huu wa viongozi wao ulichangia katika jamii hii kuathiriwa na njaa kwa sababu hakukuwa na watu ambao wangeshiriki katika kilimo.

| | |
|---|---|
| *Rigesa riabeire ang'e* | *Mavuno yamekaribia* |
| *Riabeire ang'e riabeire ang'e* | *Yamekaribia yamekaribia* |
| *Endagera yaamire buya* | *Chakula kimenawiri vizuri* |
| *Emegondo yaamire mono* | *Mashamba yana chakula kingi* |

Mandhari ya '*Obori Bwa Baba'* (Wimbi Jameni) pia yametumiwa kuonyesha vyakula mbalimbali ambavyo jamii hii ilkuwa inapanda na jinsi vilivyokuwa vimenawiri shambani. Kwanza taswira ya wimbi ambao umenawiri vizuri inachorwa pale ambapo wanasema kuwa wimbi huo umekodoa macho. Kutokana na wimbi, waliweza kuandaa ugali wa wimbi ambao ulikuwa unaenziwa na kila mtu. Kando na hayo ugali huu ulikuwa muhimu sana katika sherehe za ndoa kwa sababu ulikuwa ni ishara ya utamaduni wao. Pia, kupitia kwa wimbi waliweza kuandaa uji kwa sababu si kila mtu ambaye alikuwa anatumia maziwa. Hali kadhalika, tulionyeshwa jinsi ambavyo viazi vitamu vilikuwa vimekomaa na vilisubiri kuvunwa. Kwa vyakula vyao, kunywa uji wa wimi na viazi vitamu lilikuwa jambo la muhimu sana hasa kwa watu ambao walikuwa wanafanya kazi ngumu kama vile kuenda kwa shambani kwa sababu vyakula hivi viliaminiwa kuwa vilikuwa vinawapa nguvu zaidi ya kufanya kazi. Wakulima waliambiwa kuwa wanastahili kuwa makini shambani kwa sababu kulikuwa na hatari ya vyakula vyao kuvamiwa na nzige jambo ambalo lingewaletea hasara kubwa sana. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| ***Kiongozi****-Obori bwa baba matogoro* | *Wimbi wa jameni umekodoa macho* |
| *Ee matogoro obori bwa baba matogoro* | *Ee wakodoa macho wimbi wa nyanya umekodoa macho* |
| *Ee matogoro* ***x2*** *baba motegerere nyangweso ndindindi* | *Ee wakodoa macho* ***x2*** *jameni tegeeni nzige ndindindi* |
| ***Kiongoz****i-Marabwani a baba Manga nse* | *Viazi vitamu jameni Manga* |
| *Ee Manga nse marabwani a baba Manga nse* | *Ee Manga chini viazi vitamu jameni Manga chini* |
| *Ee Manga nse* ***x2*** *baba motegerere nyangweso ndindindi* | *Ee Manga chini* ***x2*** *jameni tegeeni nzige ndindindi* |

## MUHTASARI

Makala haya yaliangazia mandhari matano kupitia kwa nyimbo za jadi ambapo yamefafanua kwa kina jinsi ambapo mandhari hayo yametumiwa kueendeleza ujumbe wa nyimbo hizo za jadi. Katika mandhari ya jandoni, makala haya yalionyeshwa jinsi ambayo wavulana ambao walikuwa wanapelekwa jandoni walivyo funzwa kungwi za utu uzima. Vijana hao walikumbushwa kuwa sasa wao ni wanaume hivyo basi wajiepushe na matendo ya kitoto kama kukaa karibu na mama zao, kulia na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

kucheza. Mama zao pia walikumbushwa kuwa wasiwatume wavulana hao mtoni wali wasiingie jikoni kwa sababu hizo zilikuwa ni kazi za wanawake. Walikumbushwa kuwa walikuwa na jukumu la kuitunza jamii na hasa kuikinga kutoka kwa wizi wa mifugo kutoka kwa jamii ya Wakalenjin na Wamaasai.

Hali kadhalika, katika nyimbo za ndoa mandhari hayo yalitumiwa kuwanasihi wanandoa kuhusu maisha ya ndoa. Wawili hao walikumbushwa kuiheshimu ndo ana kuwa katika ndoa hakuna talaka. Walisisitiziwa kuwa yeyote atakayeomba au kutoa talaka angedharauliwa na wanajamii. Wanandoa pia waliambiwa umuhimu wa kupata watoto kwa sababu hii ndio njia pekee ya kukiendeleza kizazi chao. Mwisho kabisa walihimizwa washikirikiane katika kila hali ili kuijenga familia imara.

Kupitia kwa nyimbo za mbolezi mandhari hayo yalitumiwa katika kuonyesha imani ya jamii kuhusu kifo. Jamaa na wanajamii walikuwa wanakumbushwa kuwa kifo kilikuwako na kitaendelea kuwako hivyo basi ni lazima waridhie. Mandhari haya pia yalitumiwa kuendeleza taasubi ya kiume ambapo wanajamii waliamini kuwa machozi ya mwanamume hayapswi kuonekana kwa sababu kulia kwa mwanamume ilikuwa ni ishara ya unyonge. Fauka ya hayo mandhari ya kuzaliwa kwa mtoto pia yalishughulikiwa kwa kina ambapo yalitumiwa kumpongeza mama aliyejifungua salama. Jamii hii iliamini na bado inaamini kuwa kipindi cha uja uzito ni kigumu sana na ndio sababu kinarejelewa kama “kuwa juu ya mti”. Mama anapojifungua salama wanajamii wanaandaa sherehe kubwa ya kumpongeza mama huyo na kumkaribisha mtoto huyo kwenye jamii. Hali kadhalika, mandhari hayo yanatumiwa kuonyesha jinsi ambavyo jamii inamthamini mtoto wa kiume. Mtoto huyo anarejelewa kama nyota na simba. Wanajamii waliamini kuwa mtoto wa kiume akizaliwa familia hiyo itaheshimiwa na kila mtu.

Nyimbo za kazi zilitumiwa katika kusawiri mandhari ya shambai ambapo shughuli za kilimo zimeshugulikiwa kwa kina. Kupitia kwazo ilibainika kuwa jamii hii ilijushughulisha na upanzi wa wimbi, viazi vitamu, mboga na mahindi. Mbali na hayo, pia wanajamii walihimizwa umuhimu wa kutunza na kutumia mazao yao vizuri ili wasiadhiriwe na njaa. Mandhari haya pia yalitumiwa kusawiri mgogoro kati ya jamii hii na mazingira yake kama vile vyakula shambani kuvamiwa na nzige.

## HITIMISHO

Makala haya yamefafanua usawiri wa mandhari katika nyimbo teule za jadi za jamii ya Wakisii. Katika kazi hii imefanikiwa kuonyesha jinsi mandhari yanatumiwa kuendeleza tamaduni na imani za jamii, kwa mfano katika sherehe za mazishi ambapo jamii inaamini kuwa machozi ya mwanamke hayasthili kuoneka. Hali kadhalika, mandhari haya yameonyesha jinsi ambavyo mandhari yanakuza maudhui mbalimbali kama vile: mgogoro/mzozo, nafasi ya mwanamke katika jamii na hata maudhui ya mabadiliko. Mbali na hayo, mandhari yamesaidia kuelewa shughuli za kiuchumi za jamii hii na mambo ambayo yanathaminiwa na wanajamii.

## MAREJELEO

Galtung, J. (1972). *Peace by Peaceful Means: Peace and Conflict Development and Civilization*. London.

Hakola, O. (2014). *Death in Literature. Cambridge Scholars Publishing*. Columbia University.

Hasaan, O.H. (2024). *Mandhari katika Riwaya* (Haijachapishwa). Moi University

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Muusya, J.K. (2012). *Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa Diwani za Pendo la*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3020

*Heba Na Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Kenyatta University

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. (Chapa ya Pili). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press. Dar es Salaam.

Wall, A. J. (1985). *Negotiation Theory and Practice*. Glenview Scoff Foresman. Illinois.

Wamitila, K.W. (2008). *Kazi za Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: VideMuwa. Publishers Ltd

World Health Organization (24TH APRIL 2024) *Maternal Mortality*.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.